
# Ulimwengu Bila Njaa




## Kwanini baa la njaa limeendelea kuwepo,Katika ulimwengu uliosheheni?

Njaa haistahimiliki

Hali ya njaa ya ulimwengu ambayo **ilipungua** kati ya mwaka 2005-2015 imeanza kuongezeka tena tangu wakati huo;hali ya njaa ya ulimwengu

sasa iko katika viwango kama vile vya mwaka 2010.Utofauti wa kipekee katika uelekeo huu umekuwa katika Uchina, ambayo ilifanikiwa **kufuta** umasikini uliokithiri mwaka 2020.

Ripoti ya mwaka 2021 ya shirika la umoja wa mataifa(UN) la chakula na kilimo(FAO) kuhusu hali ya usalama wa chakula na lishe ya ulimwengu,*The State of Food Insecurity and Nutrition in the World*,**inabainisha** kuwa ‘takribani mtu mmoja kati ya watu watatu(yaani watu bilioni 2.37) walikuwa hawamudu kupata kupata mlo wa kutosha katika mwaka 2020-ambayo ilikuwa ni ongezeko la watu takrbani milion 320 katika kipindi cha mwaka mmoja’.

Shirika la umoja wa mataifa (UN) la mpango wa chakula (WFP) linakisia kuwa idadi ya watu wenye njaa itaongezeka mara mbili kabla janga la UVIKO-19 halijadhibitiwa na kama ‘hatua madhubuti hazitochukuliwa’.

Wanasayansi wanatuarifu kuwa hakuna uhaba wa chakula chenye kukidhi idadi ya watu:kimsigi,uwezo wa ugavi wa kalori kwa mtu mmoja*(supply of calories per capital)* **umeongezeka** ulimwenguni kote.Watu wana njaa si kwasabu tupo wengi,ila kwasababu wazalishaji wadogo katika sekta ya kilimo ulimwenguni wanaondolewa kutoka maeneo yao ya uzalishaji na *kilimo-biashara* na kulazimishwa kuelekea katika miji mikubwa ambako upatikanaji wa chakula hutegemea pato la fedha.Matokeo yake, mabilioni ya watu hawana namna ya kununua chakula.

Tafiti zote za kihistoria zinaonesha kuwa baa la njaa huwa halisababishwina upungufu wa ugavi wa chakula,isipokuwa upungufu wa nyenzo/namna ya kupata chakula.Kama ambavyo FAO waliandika **mwaka** 2014, 'uzalishaji 'wa sasa wa chakula na mifumo ya usambazaji wake inashindwa kuulisha ulimwengu.Wakati kilimo kinazalisha chakula cha kutosha kwa watu bilioni 12 hadi 14, watu takribani milioni 850-ama moja ya nane ya idadi ya watu wote duniani wanaishi katika hali ya njaa iliyokithiri'.Kushindwa huku kunaweza **kupimwa**, kwa sehemu,na hoja kuwa moja ya tatu ya chakula chote kizalishwacho kinapotea ama katika uchakataji na usafirishaji ama kinatupwa.Si idadi kubwa ya watu inayosababisha njaa kama ambavyo husemwa mara nyingi isipokuwa kutokuwepe usawa na msukumo wa kulimbikiza faida,mfumo wa chakula unaotawaliwa na kilimo biashara ambao katika huo hata mahitaji ya msingi kwaajili ya chakula cha mamilioni ya watu-kwa uchache-hutolewa sadaka kukidhi kiu ya faida ya wachache.

## Uhuru wa chakula ni nini?

Mwaka 1996 kauli mbili za lazima,usalama wa chakula na uhuru wa chakula ziliingia  katika mkondo mmoja kimjadala na tafakari.

Dhana ya uhuru wa chakala, ilitokana na mapambano ya kijamaa na mapambano dhidi ya ukoloni na kwa urasmi iliasisiwa katika Mkutano wa chakula wa ulimwengu uwa FAO(1974),inakaribiana na wazo/dhana ya taifa kujitosheleza kwa chakula.Mwaka 1996,kam sehemu ya **Azimio la**

**Roma,** dhana ya usalama wa chakula ilitanuliwa ili kuibua umuhimu wa uwezo wa kiuchumi kwa upatikanaji wa chakula, na serikali kujibidiisha kuhakikisha upatikanaji wa chakula kwa wote kupitia sera za mapato na usambazaji wa chakula.

Mwanzoni mwa miaka ya 90,dhana ya uhuru wa chakula iliundwa na **La Via Campesina**,mtandao wa kimataifa ambao leo unajumuisha wakulima wadogo milioni 200 kutoka nchi 81,kusisitiza kuwa si tu serikali zitoe chakula,lakini pia watu wajengewe uwezo kuzalisha vitu muhimu kwa chakula.

Uhuru wa chakula **ulitafsiriwa** katika la uundaji wa mfumo wa kilimo na chakula ambao utalinda 'haki ya afya kwa watu na chakula chenye kukidhi utamaduni wao kupitia njia endelevu na haki yao ya kutafsiri/kuamua chakula chao na mifumo ya kilimo'.

Takribani muongo mmoja baadaye, La Via Campesina, The World March Women, na makundi mbalimbali ya mazingira waliandaa Jukwaa la Kimataifa La Uhuru wa Chakula huko Nyèleni(Mali) mwaka 2007. Katika jukwaa walifafanua masuala ya msingi sita ya uhuru wa chakula:

1. Kuzingatia mahitaji ya watu badala ya mahitaji ya mtaji/soko.
2. Kuthamini wazalishaji wa chakula,kwa kuunda sera zinazothamini wakulima wadogo na kunawirisha maisha yao.

3. Kuimarisha mfumo wa chakula kwa kuhakikisha mitandao ngazi za chini kabisa,kikanda na kitaifainashirikiana na kuthamini wale wenye kuzalisha na wenye kukitumia chakula.Hii itaimarisha ushiriki wa wazalishaji wa chakula na walaji katika kuunda na kutengeneza mifumo ya chakula na kuhakikisha kuwa vyakula vyenye kiwango duni na visivyo salama havilundikani na kuzuia jaribio la kuunda soko la chakula lenye haki.
4. Kutumia mbinu za wenyeji za udhibiti wa uzalishaji chakula; kwa maneno mengine,kuwapa wale wazalishao chakula haki ya kutafsiri namna ya kuratibu ardhi na rasilimali.
5. Kujenga maarifa na stadi,zinazosisitiza ya kutumia maarifa ya wenyeji kuhusu uzalishaji wa chakula kwa uthabiti na kuyaendeleza zaidi kisayansi.
6. Kufanya shughuli sambamba na kuheshimu asili ili kupunguza madhara kwa mifimo ya ikolojia kupitia aina za kilimo zisizo na uharibifu kwa ulimwengu-asili.

Dhana ya 'uenyeji' inahitaji ukaguzi makini wa ngazi ya utabaka,ujamii na jinsia; hakuna 'jumuiya enyeji' ama 'uchumi enyeji' ambao haushambuliwi na unyonyaji na vurugu za ngzi hizi.Vivyo hivyo maarifa/ujuzi enyeji lazima utizamwe sambamba na ukuaji wa sayansi ya kileo,ambayo kupenya kwake katika eneo la kilimo hakupaswi kupuuzwa.

Kinacholiimarisha jukwaa la uhuru wa chakula ni mstari mkali linaouchora kujitenga na mtindo wa uzalishaji chakula wa kibepari.

Biashara na soko huria katika uzalishaji na usambazaji wa chakula inatengeneza uharibifu mkubwa.Biashara husia si tu inaleta hatari ya uingizwaji wa bidhaa za bei ya chini,ambazo zinakandamiza bei za mazao lakini pia inaleta bei zisizotabirika kwa kuingiza bei za kimataifa katika masoko ya ndani.Aina hiyo ya uhuria inahatarisha kubadilika kwa aina ya mazao yalimwayo katika nchi zinazoendelea ili kukidhi matakwa ya mataifa tajiri zaidi,hivyo kuathiri uhuru wa chakula.

Mwaka 2010,Mwandishi maalumu wa zamani wa umoja wa mataifa juu ya umasikini uliokithiri na haki za binadamu,Olivier De Schutter ,**alitoa tahadhari** kuhusu namna mifuko ya uwekezaji mitaji, mifuko ya pensheni, na benki za uwekezaji zilivyokizidi uwezo kilimo na ulanguzi kupitia uwekezaji wa bidhaa, hati fungani na hisa.Njia hizi za kifedha hazijali juu ya misingi ya masoko ya kilimo’.These financial methods, he wrote, were ‘generally unconcerned with agricultural market fundamentals’.Ulanguzi wa kifedha katika kilimo unaonesha namna gani fedha haijali msawazo katika mfumo wa uzalishaji chakula unaweza kuwanufaisha wazalishaji na walaji wote pamoja.Unahamasisha nguvu ya fedha kuharibu mfumo wa uzalishaji chakula.

Dhana ya uhuru wa chakula ni hoja dhidi ya aina hizi za uharibifu, ambazo zinakita mizizi katika **uporaji ardhi** unaofanywa na makampuni makubwa ya kilimo biashara.

Tangu karne hii kuanza,makampuni makubwa ya kilimo biashara kama vile Unilever na Monsanto yamehamasisha uzuiaji mkubwamkubwa(***land enclosure***) kwa maeneo mengi ulimwengu mzima katika zama zetu, hali iliyopelekea uhamaji mkubwa wa watu kushinda kipindi chochote katika historia na kwa kufanya hivyo kuharibu kabisa mahusiano baina ya watu na ardhi.

Maazimio mawili ya Umoja wa Mataifa-moja l**inatamka** haki ya maji(2010) na lingine **linahakikisha** haki za wakulima wadogo(2018)- yatatusaidia kuhunzi mfumo wa kilimo ambao unaweka mbele maslahi ya wazalishaji(ikiwamo haki ya kupata ardhi) na heshima kwa asili(mazingira asili) na unaofanya maji kuwa jambo la wote na sio bidhaa.

## Tunawezaje kuunda mfumo wa uzalishaji na usambazaji wa chakula ulio wa haki?

Vyombo vya wakulima wadogo vimekuza uelewa wa kutosha juu ya kushindwa kwa aina/mtindo wa uzalishaji wa chakula wa kibepari.Takwa lao la haraka ni kusimikwa mtindo wa aina nyingine,ambao unasisitiza demokrasi pana ya ushiriki katika ujenzi na uundaji wa mifumo ya

chakula,ushiriki unaohusisha ushiriki wa serikali kushinda mashirika ya misaada ama sekta binafsi.Kutoka katika matakwa yao mengi,tumechuja hoja zifuatazo:

1. Kugatua nguvu ya uchumi kwa watu kwa:
    - Kutekeleza mageuzi ya kilimo(agrarian reform) kwa wakulima wadogo na wakulima ili wamudu kupata ardhi na rasilimali kwaajili ya kufanya kilimo
    - Kutengeneza miundo inayofaa ya uzalishaji inayohamasisha pamoja na mambo mengine-jitihada za pamoja ili kupata manufaa ya uchumi kwa skeli kubwa.
    - Kuunda mamlaka vijijini ambapo wakulima wadogo watakuwa na ngucvu ya kisiasa inayomudu kushawishi sera zenye kunufaisha maisha yao huku zikilinda mfumo wa ikolojia.
    - Kuimarisha mifumo ya huduma za ustawi jamii(social welfare) ili wakulima wadogo walindwe katika nyakati ngumu(hali mbaya ya hewa,mavuno hafifu n.k)
    - Kujenga mifumo ya usambazaji ya umma, yenye lengo mahususi la kuondoa njaa.
    - Kuhakikisha kwamba chakula salama*(healthy food)* kinapatikana katika taasisi za elimu za umma na vituo vya malezi ya watoto.

2. Endeleza na tekeleza hatua zinazohakikisha kilimo kina tija***:***

- Kuzuia uingizwaji(kugeuzwa jaalala) wa bidhaa za vyakula za bei nafuu toka mataifa yaliyoendelea(Global North) ambazo zinufaikana ruzuku nyingi.
- Kutanua wigo kwa wazalishaji vijijini kupata mikopo himilifu na kupewa nafuu toka kwa wakopeshaji wasiokuwa rasmi.
- Kuunda sera kuhakikisha bei nzuri(*floor prices*) kwa mazao ya mashambani.
- Kuuunda skimu endelevu za umwagiliaji,mifumo ya uchukuzi,vifaa na maeneo ya kuhifadhi mazao na miundombinu inayofanana na hiyo, iliyo ya umma.
- Kuipa nguvu sekta ya ushirika katika kuzalisha chakula na kuhamasisha ushiriki wa umma katika mifumo ya uzalishaji chakula na usambazaji chakula.
- Kujenga uwezo wa kisayansi na teknolojia endelevu na kilimo cha kiikolojia.
- Kuondoa hati miliki kwenye mbegu na kutengeneza miundo ya kisheria inayolinda mbegu za asili zisibidhaishwe na kilimo-biashara.
- Kutoa pembejeo za kilimo za kisasa kwa gharama nafuu.

3. Kusanifu mfumo wa kidemokrasia wa kimataifa wa biashara kwa:

- Kulifanya shirika la biashara la kimataifa kuwa la kidemokrasia,jambo linalohusisha:

i. Ushiriki mpana zaidi na wa makusudi wa nchi za Kusini katika kuunda kanuni,uwazi zaidi katika katika michakato ya mijadala ya makubaliano(ikiwamoikiwamo taarifa na jumbe za mijadala ya makubaliano), na ushiriki wa vyombo vya wakulima wadogo katika mchakato wa uundaji kanuni.
ii. Uwazi mkubwa zaidi katika suala la migogoro ya kibiashara.Hii inahusisha utangazaji wa mgogoro wowote na kwa wakati na aina  ya suluhu pamoja na kutangaza kwa umma juu ya maamuzi ya kimahakama.

- Kupunguza utegemezi kwa majukwaa yenye nguvu ya nchi za kaskazini(Global North) kanika kusanifu sera na kutatua masuala;hii inajumuisha Shirika la  Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo na Kituo cha kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji cha Benki ya Dunia.Vyombo hivi vinadhibitiwa na nchi za Kaskazini, na vinafanya kazi moja kwa moja kwaajili ya  ustawi  wa makampuni makubwa ya kimataifa.

Imetafsririwa na; **Muhemsi  C. Mwakihwelo**